

Katika ulimwengu ambao hisia tamu na zenye ushawishi mkubwa ni hisia za mapenzi.....

Kuna mambo mengi machungu huweza kutokea wakati wa kutafuta utamu huo wa kupendwa na kupenda.

Kuna mambo yanaweza kutokea pale watu wawili wanaosema wanapendana wanapokubari kwenda kwenye safari inayowahusisha wao wawili tu, bila kuwa na wasaidizi wala mashahidi.

Kwa sababu wanaaminiana.

Haswa huo ndio msingi mkubwa wa mahusiano.

Uaminifu ni nguzo muhimu mno ya mahusiano.

Bila uaminifu wakati wowote tutegemee mahusiano kuvunjika.

Sasa mtu unapogundua au kuhisi kwamba mwenzi wako anakusaliti au amekosa uaminifu ni moja ya hisia ya kuumiza mno mtu kuwahi kuhisi.

Maumivu hayo ya kihisia yanaweza kukupelekea kwenye maamuzi ya kudhuru au kujidhuru wewe binafsi.

Hatimaye ukaacha msiba mkubwa kwa wengi wanaokupenda na kukutegemea kama mtu wa muhimu kwao.

Vitu kama hasira na huzuni ni hatari kwa afya ya moyo wako. lakini huwenda kuna vitu vinyavokusababishia hizo hali.

Vitu hivyo vinakuachia maswali kichwani ambayo majibu yake hata hujui utayapata wapi.

Umekumbwa na msongo wa mawazo, kila ukikumbuka viapo na makubaliano mliyoyafanya huko nyuma basi unajihisi umepoteza kila kitu.

Kuchiti au usaliti si kitu kidogo tunapokiongelea hasa kwenye ndoa au mahusiano, ambayo mmoja wa wahusika aliweka juhudi kubwa na kutarajia makubwa.

Kuna watu hutumia mahusiano kujinufaisha wao binaffsi, aidha kwa kujiridhisha kihisia au kimahitaji mengine kama fedha n.k.

Hii inaweza kupelekea mmoja wa muhusika wa mahusiano kuonekana kama mjinga fulani hivi aliyekosa kitu cha kufanya.

Lakini haitokuwa hivyo kwako kwa sababu dakika chache zijazo ninakwenda kukufunulia siri nzito iliyojificha ndani ya mchezo huu wa kucheat.

Kuna dalili ambazo ukiziona na kuzithibitisha kwa mtu wako angarau zaidi ya tatu ni lazima mtu huyo atakuwa anakuchiti.

Lakini pia kuna namna ya kukabiliana na hali hiyo endapo ikikukabili.

Hapa hapahitaji hasira ila nitakupa hekima za kukusaidia zaidi wewe ili usiathirike zaidi.

Katika hiki kitabu utakwenda kujifunza njia za kufanya endapo ukakutana na changamoto hii kwenye mahusiano yako.

Nitakufundisha kwa mapana yake namna ambavyo kuchit kunafanya kazi na wewe ujiokoaje kwenye changamoto hiyo.

Natamani mwisho wa kusoma kitabu hiki upate tumaini jipya ya namna ya kutatua changamoto zako za mahusiano